

(17). Bahlul Na Mwizi Wa Viatu.

Siku moja Bahlul alikwenda Msikitini akiwa amevaa viatu vipya, na huko alimuona mtu mmoja akiviingalia mno viatu vyake, hivyo akaelewa kuwa ataweza kuviiba.

Basi Bahlul akavichukua viatu vyake na kuviweka mbele yake huku akisali.

Yule mwizi akamwambia: "Sala haisihi katika hali hiyo!"

Bahlul akamjibu: "Iwapo sala itanitoka basi viatu vitabaki."